SUMAIT Journal (SJ)
eissn (e- ISSN2953-2698)
Issue No.13 Decembar 2023

# Nduni za Utanzia katika Riwaya za Kiswahili: Mshabaha Baina ya Haini na Rosa Mistika

**Haji Khatibu Ali**
**Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA)**
Swahibaali@ gmail.com

*Received: June 2023, accepted: 30 Agust 2023, Published: December 2023*
*© SUMAIT Journal 2023*

**Abstract:**

*A distinctive feature of some works of Swahili literature of twenty – first century is the extensive use of experimental writing methods (Mwamzandi, 2013:48). Over the years, Swahili literature has been portraying the society in accordance with the reality that is accompanied by tragic. It is considered that there has not yet been sufficient research done on the topic which has caused a burden and strangeness among the readers. In order to avoid this challenge, this paper intends to investigate this literary technique for the sake of bringing a wider understanding while its elaboration focused on clarifying its characteristics according to the pens of two writers who were born and raised in different environments. They are Adam Shafi (Traitor, 2003) from the island of Unguja in Zanzibar and Euphrase Kezilahabi (Rosa Mistika, 1971) a native of Ukerewe island in Tanzania Mainland. The Reception theory whose founder is Rosenblatt (1938) has been used in this research. It is the theory that emphasizes the role of the reader and discards the role of the author in interpreting literature. Library reading (documentation) technique was used in data collection. At the same time the descriptive method has captured the research for analytical target. The result of the investigation has shown that there are distinctive features based on tragic novels.*

**Keywords:** *Tragic Novels, Swahili Novels, Haini (Traitor), Rosa Mistika*

## Ikisiri

*Sifa bainifu ya baadhi ya kazi za fasihi ya Kiswahili za karne ya ishirini na moja ni matumizi makubwa ya mbinu za kiuandishi za kimajaribio (Mwamzandi, 2013:48). Miaka nenda rudi, fasihi ya Kiswahili imekuwa ikiing'ongona jamii kuendana na uhalisia unaolandanishwa na utanzia. Huku ikizingatiwa kuwa bado utanzia haukufanyiwa uchunguzi toshelevu kiasi ambacho husababisha kuelemewa na ugeni masikioni mwa wasomaji. Ili kuepukana na changamoto hii, makala imenuia kuichunguza mbinu hii kwa minajili ya kuleta uwelewa mpana huku ufafanuzi wake ukijikita kuweka wazi nduni zake kulingana na kalamu za waandishi wawili waliozaliwa, kulelewa na kukulia katika mazingira tofauti. Mmoja akiwa ni Adam Shafi (Haini, 2003) anayetoka kisiwa cha Unguja Zanzibar na Euphrase Kezilahabi (Rosa Mistika, 1971) mwenyeji wa kisiwani Ukerewe Tanzania Bara. Nadharia ya Upokezi imetumika katika utafiti huu ambayo iliasisiwa na Rosenblatt (1938). Ni Nadharia inayoweka mkazo nafasi ya msomaji na kutupilia mbali nafasi ya mtunzi kutoa tafsiri ya fasihi. Mbinu ya usomaji wa maktabani (nyaraka) ilitumiwa katika kukusanya data. Wakati huo huo njia ya maelezo imeuteka utafiti kwa shabaha ya kiuchambuzi. Matokeo katika utafiti huu yalionesha kuwa kuna nduni bainifu zinazojikita kwenye riwaya zenye utanzia ndani yake.*

**Keywords:** *Nduni za Utanzia, Riwaya za Kiswahili, Haini na Rosa Mistika*

## 1.0 Utangulizi

Hapana ubishi utanzia umetokana na dhana kongwe ya tanzia. Dhana ambayo imekuwa ikitumiwa kwa miongo mingi katika uga wa fasihi ya Kiswahili. Akiandika mwaka 350 K.K, mwanafalsafa wa Ugiriki wa kale Aristotle katika Daiches (1981) na Wafula & Njogu (2007:30) wanaeleza kuwa tanzia ni maigizo yenye matukio na ujumbe mzito unaowasilishwa kwa lugha inayonawiri ili kuzindua hofu na huruma na hatimaye yaripue hisia za ndani kutoka nafsini mwa hadhira. Fasihi kupata mtekenyo wa mabadiliko katika utunzi ni kitu kisichoepukika kwa sababu maisha ya binadamu hubadilika kila uchao (Jumanne & Khamis, 2021:1). Kimsingi mabadiliko hayo yamo katika kuepusha kupooza na kushindwa kushawishi kwa fikra na umbuji (Khamis, 2007:13). Ili kuuepushisha katika hatari ya kupooza ndipo baadhi ya watafiti wameivalia njuga, kuchunguza na kushawishi katika mazingira ya kuachana na istilahi ya tanzia na badala yake kuja na istilahi mpya ya utanzia.

Kwa mujibu wa Ponera (2014: 20 – 21) utanzia ni mbinu kinyume cha ufutuhi. Ni mbinu ambayo mtunzi hutumia vipengele mbalimbali vizuavyo huzuni, masikitiko, jitimai na mateso kwa hadhira yake. Vipengele hivyo huweza kujengwa na mateso, ugumu wa maisha, vifungo, mabaa kama njaa, gharika, kimbunga, magonjwa, ulemavu wa viungo au michakato ya mwili, pamoja na ule wa mifumo ya mwili kama vile ugumba, utasa. Kwa upande wake Ali (2015:5) anaeleza kuwa, utanzia una maana ya maneno, matendo, matukio au mazingira yoyote yenye kuifanya hadhira ihuzunike. Wakipigilia msumari zaidi, Said na Taid (2019:73) wanadokeza kuwa utanzia ni hali ya kutokea matukio katika

kazi ya kifasihi na matukio hayo yakamletea shida, hofu, mashaka, woga na masikitiko msomaji wa kazi husika.

Kwa kuzingatia mawazo ya fasili zote hizo kwa ujumla, makala hii inaonesha kuwa utanzia ni mbinu ya kibunulizi ilengayo kuiteka na kuiathiri hadhira kujihisi huzuni, kujawa na woga pamoja na kuingiwa na huruma. Kwa mapana na marefu utanzia unajumuuisha mambo yote yasiyoifurahisha hadhira ambayo humletea majonzi, masikitiko na msononeko wa maisha. Kwa kutumia istilahi ya utanzia, kwa hiyo katika makala hii utanzia unajadiliwa kama dhana yenye sifa muhimu zifuatazo:

1) Utanzia ni kinyume cha ufutuhi
2) Utanzia ni miongoni mwa mbinu ya kibunulizi
3) Utanzia unajengwa kwa vipengele vyenye sifa maalumu
4) Utanzia unatoa hisia za msingi za huzuni, huruma na hofu
5) Utanzia una uwezo wa kupenya na kuathiri akili au mwili wa hadhira lengwa
6) Utanzia unajidhihirisha kiusemi, kimatendo au kimuktadha

Ni mtazamo wetu suala la utanzia halijashughulikiwa ipasavyo katika ufafanuzi wa kitahakiki kama inavyosawiriwa na riwaya teule. Hii imeambatana na hoja kwamba kazi nyingi za kifasihi hubebeshwa ufundi wa kisanaa kupitia mbinu kadhaa miongoni mwazo ni hii ya utanzia. Huku ikizingatiwa kuwa kila kionjo kina upekee wake wa kutunzi na kitabia. Hivyo basi katika makala hii, tunajaribu kueleza kwa ufupi nduni muhimu za riwaya zenye utanzia. Tukisaidiwa na ufafanuzi wenye kuzingatia mifano kutoka riwayani.

### 1.1 Riwaya Teule kwa Muhtasari

Riwaya ni mojawapo ya utanzu muhimu wa fasihi ya Kiswahili. Umuhimu wake unaonekana kwenye sifa ya kuchukua mawanda mapana ya masimulizi. Kupitia riwaya mtunzi hupata ufaraguzi wa kubuni vitushi mseto ikilinganishwapo na utanzu wa ushairi na tamthiliya. Ukweli usiopingika asili ya neno riwaya linatokana na lugha ya Kiarabu رواية "*Riwiyah*" likiwa na maana ya masimulizi (Makram – Ibn Manzur:1997:153). Hata hivyo, *Atlas Encyclopedic Dictionary English Arabic* (2003:855) inadokeza روايه : قصة نثريه طويلة yaani riwaya ni hadithi ndefu ya kinathari.

Huku hayo yakijiri, riwaya haikuepuka kuelemewa na mpishano fulani wa wanazuoni wa hapa na pale juu ya maana. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999:35) riwaya ni utungo mrefu wa kubuni

wenye ploti unaotumia lugha ya nathari. Naye, Senkoro (1987:73 – 74) ana mtazamo wa kwamba riwaya ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kitambe na kutambaa mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwandishi wake. Kama hiyo haitoshi, Nkwera (1978:109) anaeleza kuwa riwaya ni hadithi iliyo ndefu kuweza kutosha kufanya kitabu kimoja au zaidi. Kwa maneno mengine, hizi ni hoja za kisayansi zenye kujipika na ambazo zinaipa riwaya uwanja mpana kuhusu ufaraguzi wa ubunifu wa matukio, uchoraji wa wahusika na matendo ya aina tofauti kulingana na muktadha.

### 1.1.1 Riwaya ya Haini kwa Muhtasari

Ni riwaya ya nne katika mfululizo wa kazi za Adam Shafi. Riwaya hii imetungwa na kuchapishwa 2003 yenye kuchukua mwelekeo wa fasihi ya ufungwa[1]. Hii ni sawiya kusema kuwa kiasi kikubwa cha hadithi kimejikita kuzungumzia maisha ya gerezani ikilinganishwa na yale machache yasimuliwayo nje ya gereza. Hii ni hadithi inayotupia jicho historia ya maisha ya Zanzibar hususani baada ya Mapinduzi ya tarehe12 Januari, 1964. Tukio kubwa lililohusishwa na historia hiyo ni mauaji ya 1972 ya Abeid Aman Karume ambaye alikuwa Raisi wa kwanza wa Zanzibar. Hii ni kama mbinu ya mtunzi katika kufichua masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Katika hatua nyingine, masimulizi ya riwaya yamegawanywa katika sehemu kuu nne. Sehemu ya kwanza inazungumzia tukio la mauaji ya kiongozi wa juu Zanzibar, aitwaye Kigogo. Sehemu ya pili inahusisha usombaji na ukamataji wa wananchi kiholeholela kwa tuhuma za kutekeleza mauji ya kiongozi huyo. Sehemu ya tatu, inayasawiri maisha halisi ya ndani ya gereza. Ni katika eneo hili ambalo riwaya inafichua siri zilizofichama magerezani. Kwa mfano, ukosefu wa haki za kibinadamu, ukosefu wa huduma za msingi kama chakula, matibabu na malazi, ukatili na udhalilishaji. Mwishowe, riwaya inaugeukia mfumo wa mahakama kwa njia ya kuukejeli na kuonesha namna ulivyopwaya katika utoaji wa haki. Mfano mzuri mahakimu wa mahakama kutobobea katika elimu ya sheria.

### 1.1.2 Riwaya ya Rosa Mistika kwa Muhtasari

[1] Ni aina za uandishi ambazo si utungaji tu wa ndani ya gereza au nje ya gereza lakini pia, zinazohusu gereza. Fasihi ya gerezani inazingatia hali halisi au ya kubuni ya mazingira ya ufungwa (Harlow, 1992:4). Masimulizi ya ufungwa ni kama utunzi kwa njia ya maneno na maelezo, yaliyoandikwa au kusimuliwa, yawe ya kubuni au si ya kubuni, yaliyotungwa ndani au nje ya gereza na ambayo yanaakisi maisha au taswira ya gereza (Walibora, 2013:11)

Riwaya hii ndiyo ya awali kutungwa na Euphrase Kezilahabi. Ilichapishwa kwa mara ya kwanza 1971 na matbaa ya *East African Literature Bureau*. Anuani ya *Rosa Mistika* inatokana na muhusika mkuu aitwaye Rosa Mistika au Rosa. Sehemu kubwa ya hadithi inahusu maisha ya Rosa tangu akiwa mtoto, makuzi ya maisha yake hadi kifo chake. Wamitila (2002:16) anasisitiza kuwa kisa cha Rosa Mistika kina mpangilio unaoakisi mfuatano wa kiwakati: maisha ya nyumbani, shuleni, chuoni, maisha ya ualimu na kifo chake. Katika masimulizi ya kisa hiki mkazo umewekwa kwenye malezi ya watoto. Riwaya inazitupia lawama asasi mbalimbali zinazohusika na malezi kama familia, shule, vyuo na mamlaka za serikalini. Hii inatokana na kutotilia maanani wajibu wa kukilea vyema kizazi. Kikubwa kinachohofiwa na mtunzi ni matumizi mabaya ya njia za malezi. Kwa mfano, kuwepo matumizi ya nguvu kubwa inayofuatana na ukali pamoja na vitisho ndani yake. Wahanga wakubwa wanaotajwa katika kadhia ya kupuuzia au kutumia njia zisizo mujarabu za malezi ni Mzee Zakaria, shuleni kwa akina Flora, Mkuu wa Wilaya na Mwalimu Mkuu Albert.

## 2.0 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti wa makala hii uliongozwa na Nadharia ya Upokezi. Rosenblatt (1938) ni mmojawapo wa wasomi wakuu waliochangia pakubwa katika Nadharia hii. Wengine waliofuatia baadae ni pamoja na Wolfgang Iser (1926 – 2007), Roland Barthes (1915 – 1980) na Stanley Eugene Fish (1938 hadi sasa). Nadharia hii iliibuliwa katika juhudi za kupinga mkondo wa uhakiki wa kazi za kifasihi kwa kumuangalia mtunzi na matini. Baadhi ya Nadharia zilizotoa kipaombele za kuihusisha kazi ya sanaa kati ya mtunzi na matini ni pamoja na Umuundo, Umuundo Sasa, Udenguzi, Umaumbo, Simiotiki/Umatini na Uhalisia (Barthes, 1977). Badala yake mkabala huu wa Mwitiko wa Msomaji unasisitiza fasihi ihakikiwe kuzingatia kigezo cha msomaji na matini. Fish (1972) anapendekeza kuwa kazi ya fasihi inakuwa halisi kuhakikiwa, endapo udurusu wa matini utafanyika ipasavyo na ambapo msomaji huboresha mitazamo, mawazo na uthaminisho wa maana kulingana na tajiriba za msomaji. Ni katika mazingira haya, Nadharia hii imemwezesha mtafiti kugundua nduni mbalimbali za utanzia kama zilivyojitokeza katika riwaya teule hasa baada ya kuzitalii kiundani.

## 3.0 Mbinu na Uchambuzi wa Data

Makala hii imelenga kubainisha nduni za utanzia katika riwaya za Kiswahili kwa kutumia vitabu vya *Haini* (2003) na *Rosa Mistika* (1971). Mbinu ya usampulishaji iliyotumika katika makala hii ni ya kukusudia ambayo humpa mtafiti uhuru wa kuteua sampuli anayotaka kwa ajili ya kupata data

(Maina, 2012). Kwa hivyo, riwaya hizi ziliteuliwa kutokana na uchunguzi wa awali uliofanywa na mtafiti kuonesha kuwa zina sifa za kipekee zinazoendana na mada na lengo la utafiti. Miongoni mwa sifa hizo ni riwaya maarufu katika jamii za Uswahilini ambazo zinaakisi utamaduni wa Waswahili. Pia, zina matukio mengi ya kitanzia yaliyotoa picha kamili ya nduni za utanzia. Namna hii, inatia nguvu kuwa nduni zilizobainika ni zenye ukubalifu hata kama zitachunguzwa kwenye riwaya nyingine zenye utanzia. Kwa upande mwingine, njia ya udurusu wa maktabani imetumika ipasavyo tangu mwanzoni hadi mwisho wa vitabu. Ni mbinu inayomtaka mtafiti kukusanya taarifa kwa umakini baada ya kusoma kwa kina kazi husika kuanzia mwanzo hadi mwisho (Enon,1998). Katika uendeshaji wa mbinu hiii, riwaya zote zilisomwa kwa umakini mpaka pale tulipojiridhisha kuwa hadithi zimeeleweka. Huku yakinukuliwa matukio ya kitanzia ambayo ndiyo yaliyowezesha kugundulika kwa nduni husika. Mkabala pekee uliotumika katika makala hii ni wa kimaelezo uliokita kufanya uchambuzi wa data zilizopatikana. Kama ambavyo Mugenda na Mugenda (1999) wanavyosisitiza kwamba utafiti wa kimaelezo unaweza kufanywa maktabani. Sehemu ifuatayo imeeleza kwa kina matokeo ya utafiti na uchambuzi wa data husika.

## 4.0 Matokeo ya Utafiti na Uchambuzi wa Data

Kuhusu hoja ya ulinganisho wa kazi za kifasihi ambayo ndiyo kiini cha mjadala wa makala hii, Jilala (2016:140) anatufumbua macho kwa kueleza kuwa:

> *Mwanafasihi linganishi analinganisha vipengele vya fani na maudhui alivyovibainisha katika hatua ya uchambuzi…anatakiwa kueleza sababu ya kufanana na kutofautiana kwa kazi hizo na kuonesha ushahidi wa kisayansi unaothibitisha kufanana ama kutokufanana kwa kazi hizo.*

Si jambo la ajabu hata kidogo mijadala ihusuyo mifanano au utofautiano, kuchukua nafasi na kupewa kipaombele katika uga wa fasihi. Pamoja na ukweli huu, makala hii haijaipa kisogo fursa hii aushi yenye kuangazia mshabihiano baina ya riwaya mbili tofauti, kwa lengo la kuipa nguvu dhana ya utanzia katika utokeaji wake. Ukubalifu wa kauli ya Jilala inaungwa mkono kwa urahisi tunapoutazama mshabaha wa utanzia ambao ulibaini sifa za msingi zifuatazo:

### 4.1 Uakisi wa Vifo

Kimojawapo cha vipengele chenye mshabaha katika riwaya ya *Haini* na *Rosa Mistika* ni matumizi makubwa ya vifo. Kwa mujibu wa Descartes (1991), kifo ni matokeo ya kutenganishwa baina ya mfumo wa roho na mwili. Becker (1971) kwa upande wake anaamini kuwa mzizi wa kifo upo kwa

madhumuni ya kujenga mienendo ya hofu na wasiwasi kwa watu binafsi au jamii kwa ujumla. Kwenye riwaya zote mbili waandishi wametumia mazingira ya vifo kama ni mbinu ya kuwaogopesha au kuwahuzunisha wasomaji. Kwa mfano katika riwaya ya *Haini* ukurasa wa 42 – 43, Adam Shafi anakieleza kwa njia ya majonzi kifo cha Kidau ambaye alikufa kwa mauaji yaliyotekelezwa na askari wa gereza. Ni kifo ambacho kilimwacha Hamza katika wasiwasi na fadhaa kutokana na urafiki wa karibu uliopo baina yao. Na kubwa zaidi linalosikitisha ni askari hao kumfungia Hamza chumbani akiwa pamoja na maiti iliyouawa kikatili. Hata hivyo, katika ukurasa wa 91 Euphrase Kezilahabi anavitaja vifo vitatu vya familia moja vilivyotokea siku moja. Ni kifo cha Mzee Zakaria baba wa Rosa, kifo cha Regina mama wa Rosa na kifo cha Rosa Mistika. Vifo vyote hivi vilimweka Honorata katika simanzi kubwa kiasi ambacho kilimsababisha kuzimia. Zaidi ya hilo, kijiji chote cha Namagondo kilikumbwa na masikitiko ya kuondokewa na wakaazi wenzao. Huku ikielezwa kuwa katika kijiji hicho hakujawahi kutokea vifo vitatu mfululizo kwa siku moja ndani ya familia moja.

**4.2 Uakisi wa Vilio**

Jambo jengine dhahiri katika kazi hizi mbili za *Haini* na *Rosa Mistika* ni kuwepo kwa matumizi mengi ya vilio vinavyoambatana na utoaji wa machozi. Kilio ni sauti yenye kuakisi hisia nzito za hasira, huruma, maumivu, msiba, huzuni au kutoridhika na jambo (BAKIZA, 2010). Akieleza juu ya nafasi ya machozi katika kilio, Mwanabaiolojia Hasson (2009:363) anafafanua kuwa machozi yenye hisia yanakusudia kuonesha nguvu ya huzuni iliyotanda katika uso wa mwanadamu. Katika riwaya ya *Haini* ukurasa wa 30 – 31, mwandishi anakihadithia kisa cha Nassor kuangua kilio kama mtoto mdogo kilichoambatana na mayowe pamoja na maombolezo kama Wooooo! Wooooo!, “Masikini mke wangu!, Masikini mwanangu!, Wooo! Wooo!”. Huku ikikumbukwa kuwa machozi yake yalikuwa mengi kiasi cha kuenea ndevuni hadi kifuani. Sababu iliyomfanya alie sana ni kuwemo katika mazingira mapya ya gerezani na akitambua sasa yumo ndani ya dimbwi la mashaka na mateso. Katika *Rosa Mistika* ukurasa wa 65, mwandishi anaweka wazi juu wingi wa machozi ya Rosa kiasi cha kujaza kikombe cha chai. Ni kilio kilichotokana na kupewa taarifa ya kufukuzwa shule. Kitendo hiki kilimuhuzunisha sana na kumuudhi vilevile. Hali iliyomfanya Mkuu wa shule kumwonea huruma Rosa, ingawa yeye ndiye aliyeiandika barua inayotoa wito wa kufukuzwa kwake

.

### 4.3 Uakisi wa Mateso

Mwanasosholojia Wilkinson (2005) anakiri kuwa elimu ya Sosholojia daima inahusika na sababu na matokeo ya mateso ya binadamu. Kwa maoni yake, anadai kwamba mateso ni tukio lisilofurahisha au ni lenye uchungu ambalo humuathiri mtu katika kiwango cha kisaikolojia na kiwiliwili. Anaendelea kueleza kuwa kupitia mateso mtu huweza kupata maumivu makali katika baadhi ya viungo vyake. Kunakomsababisha kukosa kukaa, kutembea na kulala vizuri. Katika mazingira kama haya, wote Adam Shafi na Euphrase wamekuwa mstari wa mbele kuyashihidisha mateso ambayo huibusha huzuni, huruma na hofu kwa msomaji. Mathalani, ukurasa wa 40 – 41 Adam Shafi anayasawiri mateso ya Hamza ya kuvishwa kitanzi shingoni huku akibururwa kama ngombe aliyevishwa shemere. Askari wa magereza waliivuta kamba iliyombana sawasawa shingoni na mwishowe walimpandisha juu ya kiti halafu wakakipiga teke kiti. Matokeo yake Hamza akawa ananing'inia na kutoka damu, denda na mikojo. Mateso mengine yaliyobainishwa na Adam Shafi ni kutosa na kuopoa ndani ya maji na kuingiza tambara mdomoni (Uk, 66), uwekaji wa mahabusu uchi karibu na tanuri (Uk 86) na udidimazi wa shazia ndani ya kucha za vidole, (Uk 153). Sawiya na Euphrase Kezilahabi katika ukurasa wa 7 anayeyalandanisha mateso ya Mzee Zakaria kwa mwanawe Rosa. Mzee Zakaria anatumia mtindo wa kumkaba koo Rosa hali iliyomsababisha macho yake kuwa mekundu na ulimu kumtoka nje kutokana na maumivu makali aliyoyapata.

### 4.4 Uakisi wa Mabalaa na Maafa

Wajihi wa mabalaa au maafa upo kwenye matukio yasiyotarajiwa kutokea kwake, ambayo huharibu mfumo wa kawaida katika jamii na kusababisha kupoteza uhai, kujeruhi na uharibifu wa mali pamoja na mazingira yake. Aidha, maafa hutokana na majanga mbalimbali yakiwamo mafuriko, ukame, vimbunga, milipuko ya volkano, mawimbi ya bahari na matetemeko ya ardhi, ambayo husababishwa ima na matukio ya kimaumbile au yasababishwayo na binadamu (Birkmann, 2014). Ukweli ni kwamba haya yote pindi yanapojiri katika maisha ya bunadamu, huenda akawa mhanga wa hofu na mtanziko na hivyo anajikuta katika usumbufu. Kama ilivyojitokeza katika *Haini* ukurasa wa 89, ambapo Adam Shafi anaonesha balaa la njaa na kamatakamata inavyowatesa jamii ya Wazanzibari. Balaa ambalo limewajengea wasiwasi watu iliyoendana na ukosefu wa vyakula muhimu kama sukari na mchele. Sifa za matumizi ya mabalaa pia zimo katika *Rosa Mistika* ukurasa wa 67. Mwandishi anatumia balaa la mvua kali katika giza totoro lililofungamana na dhoruba kubwa, radi pamoja na upepo mkali. Katika balaa hili liliwajengea hofu na masikitiko wakaazi wa Morogoro hasa mapaa ya nyumba zao kupeperushwa na upepo.

### 4.5 Uakisi wa Ufungwa

Suala la ufungwa au mahabusu hupatikana sehemu ya gerezani. Kulingana na *Encyclopedia Americana* (1977:619) gereza ni mahali ambapo washukiwa wa uhalifu wanamofungiwa wakingojea kufikishwa mahakamani, au ni mahali wahalifu hufungiwa kama njia ya kuwaadhibu. Neno ufungwa au mahabusu linapotajwa, fikra za walio wengi hujielekeza kwanza katika maisha ya dhiki, mashaka na katika hali ya kukata tamaa. Aidha, ni sehemu ambayo uhuru wa mfungwa au mahabusu huwekwa rehani huku akidhibitiwa kimwili, kiakili na kiroho masaa yote ishirini na nne chini ya mamlaka za kidola. Siku zote mfungwa ni mtu anayewekwa kizuizini huku akishuhudia madhila na machungu kemkemu yanayomsibu wakati wa kukitumikia kifungo chake. (Said & Taib, 2019). Katika *Haini*, Hamza na wenzake wamekamatwa na kurundikwa gerezani kwa jumla ya miaka miwili hadi mahakama inapotoa uamuzi juu ya kuhusika au la. Hamza na baadhi ya wenzake wanaachiliwa huru kwa ukosefu wa ushahidi uliohusishwa na mauaji ya Kigogo. Baadhi ya wale washukiwa walihukumiwa kifo na wengine walihukumiwa kifungo cha miaka kumi na mitano kama njia ya kuwaadhibu. La kusikitisha zaidi, pale ambapo Edi mwanafunzi wa shule kuwekwa mahabusu na kupoteza masomo yake ya *Chemistry* na *Physics*. Hii ilimfanya kujawa na huruma moyoni akikaribia kutokwa na machozi (Uk 199 – 200). Katika *Rosa Mistika* ukurasa wa 40, Deogratias anaingizwa gerezani na kupita siku mbili bila kusikilizwa kesi yao. Waliingizwa ndani ya chumba ambacho ni kidogo sana kikiwa na dirisha moja. Upande mwingine wa chumba mlikuwa na blanketi moja lenye madoadoa mengi meusi.

### 4.6 Uakisi wa Maradhi na Ugonjwa

Suala la ugonjwa ni mojawapo ya vipengele muhimu viletavyo huzuni kwa jamii. Hii ni kwa sababu ugonjwa huharibu michakato ya mfumo wa viungo vya mwili (Ponera, 2014: 20 – 21). Kwambai na Wenzake (2020) wametafiti na kugundua kuwa katika kazi za kifasihi hujenga hofu na usumbufu unaosababishwa na magonjwa ya aina mbalimbali likiwamo la UKIMWI. Kupitia data iliyopatikana imebainika kuwa riwaya za *Haini* na *Rosa Mistika* zimetumia baadhi ya magonjwa kama nyenzo ijengayo utanzia. Kwa mfano, Adam Shafi katika ukurasa wa 178 anataja maradhi ya homa, kifua na surua yalivyomwandama mtoto wa Hamza. Maradhi ambayo yamemsababishia mkewe kuwa katika hali ya udhia na majonzi. Kwa upande wa Euphrase Kezilahabi katika ukurasa wa 87 ameusawiri ugonjwa mbaya uliopewa majina mengi. Kutokana na kutia hofu katika jamii, ugonjwa uliitwa kwa

majina tofauti kulingana na eneo. Kwa mfano, Usukumani uliitwa magunia, Musoma uliitwa funyafunya na Ukerewe uliitwa miguu. Kezilahabi anaeleza kuwa maumivu ya ugonjwa huu huanzia kifuani, halafu huteremkia mgongoni mpaka magotini. Hatimaye, mtu hukosa nguvu, huanguka chini; na kama asipofikishwa hospitali kabla ya saa mbili anapoteza maisha.

### 4.7 Uakisi wa Vipigo

Mjadala kuhusu vipigo vya hapa na pale unakusudia kuthibitisha kuwa, pamoja na mambo mengine, hufanya kazi ya kuleta huzuni, woga au huruma. Tunaelezwa kuwa upigaji ni tendo la kushambulia sehemu za mwili na kusababisha maumivu au majeraha kwa wengine (Mdee na Wenzake, 2011). Huu ni muktadha ambao hushirikisha vichapo vikali vitokanavyo pengine na hasira, ghamidha au chuki baina ya mtu na mtu au jamii na jamii. Mara nyingi vipigo vinatekelezwa kwa kutumia fimbo, rungu, waya, ukanda au viungo vya mwili kama ngumi na mateke. Hali inayosababisha majeraha sehemu mbalimbali za mwili zikiwamo kichwani, mikononi, magotini na miguuni. Pamoja na hoja hiyo, matukio ya vipigo kama sifa ya utanzia imechukua upenyo ndani ya bunulizi za waandishi wote wawili. Kwa mfano bila kupepesa macho Adam Shafi anasimulia ifuatavyo:

> *Nakuuliza tena. Utatia saini au hutii?" "Sitii," alijibu Sururu, amechachamaa. Wote walimrukia kwa umoja wao, wakamnyanyua wakamrusha nje kule uwajani. Walimrusha kama kinyangarika tu akatua juu ya sakafu kichali chali kichwa kikapiga chini, kikapasuka, damu ikatawanyika mwaaa! Hapo tena, aliyekufa Mungu amrehemu. Sururu akawa kinyang'anyiro, kobe. Magongo ya mpera ambayo yalikuwa ghalani kwa muda mrefu yalitolewa. Kila mtu na lake. Pu – pu pu – pu. Sururu hakusema hata "kwin!" Walimfundafunda mpaka akazirai, wakamzoazoa wakamtupilia mbali chumbani (Uk, 133).*

Pamoja na nukuu hiyo, kinachoonekana ni kinyang'anyiro cha askari wa magereza juu ya kumshambulia Sururu kwa kutumia magongo. Inaonekana wazi kuwa askari hao wametumia magongo ya mpira katika mwili wa Sururu. Ni tukio ambalo linamsababishia kupata majeraha ya kichwa yaliyofuatana na utoaji wa damu nyingi. Sawa na Euphrase Kezilahabi katika ukurasa wa 39 amelibebesha tukio la upigaji kati ya askari polisi na Deogratias. Kinachosimuliawa zaidi katika kadhia hii ni kwamba askari alimpiga makofi mawili Deogratias ambayo yalimuangusha chini na hatimaye kutokwa damu nyingi puani.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza na kubainisha nduni bainifu za utanzia katika riwaya za Kiswahili. Huku riwaya zilizoteuliwa zikiwa ni *Haini* na *Rosa Mistika* kama viwakilishi vya riwaya nyingine. Mjadala huu umethibitisha kuwa, bila kuwapo kwa matumizi kama vile vifo, vilio, mateso, mabalaa, ufungwa, ugonjwa na vipigo; ni vigumu kujengeka utanzia ndani ya bunulizi. Nduni zilizobainika ni kielelezo tosha kuwa utanzia hautokani katika ombwe bali husukwa kutokana na watunzi kuchochewa na utumiaji wa vipengele maalumu vyenye kuutambulisha utanzia. Vilevile, mjadala umethibitisha kuwa nduni hizo zinaweza kusimama kama misingi au mihimili ya kuutazama kwake. Hii inamaanisha kuwa, ikiwa mtunzi analenga kuisuka kazi yake kwa jicho la kiutanzia, anaweza kutumia nduni hizi kama nyenzo za kumwongoza au kusimamia. Kwa maneno mengine, hakuna kazi ya kifasihi ambayo haina vipengele tajwa halafu ihesabike kuwa ni miongoni mwa kazi zenye utanzia. Kwa ujumla, nduni zilizobainika ni za lazima katika kazi yoyote ya fasihi (taz. Ponera, 2014), kwani vinahusiana na kuathiriana kwa kiasi kikubwa.

## Marejeleo


- Ali, H.K. (2015). Matumizi ya Utanzia katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed. Tasnifu ya Umahiri ya Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Atlas Encyclopedic Dictionary (2003). Atlas Publishing House. Egypt.
- BAKIZA (Baraza la Kiswahili la Zanzibar). (2010). Kamusi la Kiswahili Fasaha. Oxford University Press. Nairobi.
- Barthes, R. (1977). The Death of The Author. Fontana. London.
- Becker, E. (1973). The Denial of Death. Simon & Schuster Publishers. New York.
- Birkmann, J. (2014). Measuring Vulnerability to Natural Hazards: Towards Disaster Resilient Societies. United Nations University Press. Tokyo.
- Daiches, D. (1981). Critical Approaches to Literature. Longman. London.
- Descartes, R. (1991). A Discourse on Method: Meditations and Principles of Philosophy, J. M. Dent & Sons Ltd. London.
- Encyclopedia Americana. (1979). Americana Corporation. New York.
- Enon, J.C. (1998). Educational Research Statistics and Measument: Educational Psychology. Makekere University Press. Kampala.
- *Fish, S.E. (1972). Self – Consuming Artifacts: The Experience of Seventeenth – Century Literature*. University of California Press Ltd. London.
- Hasson, O. (2009). "Emotional Tears As Biological Signals" Katika Makala ya Evolutionary Psychology. Vol, 7 (3), Uk, 363 – 370.
- Harlow, B. (1992). Barred: Women, Writing and Political Detention. University Press of New England.
- Jilala, H. (2016). Misingi ya Fasihi Linganishi: Nadharia, Mbinu na Matumizi. Daud Publishing Company Dar es Salaam.
- Jumanne, A & Khamis, T.Y (2021). "Mabadiliko ya Vionjo vya Kiuandishi katika Riwaya ya Kiswahili". Katika Ruaha Journal of Arts and Social Sciences. Juz, 7. Uk, 1 – 10.
- Kezilahabi, E. (1971). Rosa Mistika. East African Literature Bureau. Nairobi.
- Khamis, S. (2007). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili".Katika Kioo cha Lugha. No. 5. Dar es Salaam: TUKI.
- Kwambai, M na Wenzake. (2020). "Ndwele Ielekezayo kwenye Kifo katika Ua la Faraja na Kichwamaji". Katika Jarida la CHALUFAKITA. Juz, Na. 2.

- Maina, S. M. (2012). Qualitative and Quantitative Research Methods Simplified. Privately Printed at Frajopa Printers Mall. Nairobi.
- Makram (Ibn Manzur), A.J.M. (1997). Lisan Al – Arab. Dar – Sader Publisher. Beirut.
- Mdee, J. S na Wenzake. (2011). Kamusi ya Karne ya 21. Longhorn Publisher Ltd. Nairobi.
- Mugenda, O.M. na Mugenda, A. G. (1999). Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches. Act Press. Nairobi.
- Mwamzandi, I. (2013). "Riwaya Teule za Karne ya Ishirini na Moja na Udurusu wa Nadharia za Fasihi". Katika Swahili Forum. Juz, 20. Uk, 48 – 66.
- Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu. Jomo Kenyatta Foundation Ltd. Nairobi.
- Nkwera, F.V. (1978). Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo. Tanzania Publishing House. Dar es Salaam.
- Ponera, A.S. (2014). Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi. Karljamer Print Technology. Dar es Salaam.
- Rosenblatt, L.M. (1938). Literature as Exploration. Noble and Noble. New York.
- Said, Z & Taib, A.H. (2019). Fasihi ya Ufungwa Nadharia na Mikabala ya Uhakiki – Riwaya kama Kifani. Heko Publishers. Dar es Salaam.
- Senkoro, F.E.M.K. (1987). Fasihi na Jamii. Press and Publicity Centre. Dar es Salaam.
- Shafi, A. (2003). Haini. Longhorn. Nairobi.
- Wafula, R.M. & Njogu, K. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi. Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi.
- Walibora, K. W. (2013). Narrating Prison Experience: Human Rights, Self, Society and Political Incarceration in Africa. CHICAGO Common Ground.
- Wamitila, K.W. (2002). Uhakiki wa Fasihi – Misingi na Vipengele Vyake, Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.
- Wilkinson, I. (2005). Suffering: A Sociological Introduction. Polity Press. United Kingdom.